MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA

# JARIDA LA HALI YA HEWA

**Na: 26. Msimuwa Kilimo 2016/17** **Tathmini ya Kipindi cha Juni 11-20, 2017 na matazamio kwa kipindi cha Juni 21-30, 2017**

**MUHTASARI**


- Katika kipindi cha Juni 11-20, 2017, maeneo mengi nchini yalikuwa makavu.
- Mazao yamekomaa katika maeneo mengi ya nchi ambapo katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Rukwa, Katavi, Iringa, Mbeya, Njombe, Lindi, Ruvuma na Mtwara zao la mahindi lilikuwa katika hatua ya kuvunwa. Katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Tanga na Kilimanjaro zao la mahindi lilikuwa katika hatua ya kukomaa**.**
- Vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani.
- Hali ya ukavu inayotarajiwa itafaa kwa shughuli za uvunaji na uhifadhi wa mazao. Hata hivyo hali hiyo itasababisha upungufu wa maji kwa mifugo, hivyo wafugaji wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na matumizi endelevu ya maji.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2017

Katika kipindi tajwa, mgandamizo mkubwa wa hewa wa Afrika Mashariki, unaotokana na migandamizo mikubwa ya hewa iliyoko kusini mwa Bara la Africa (ST. Helena na Mascarene) iliimarika wakati ile iliyopo sehemu za kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kupungua nguvu kidogo na hivyo kuendelea kuruhusu ukanda wa mvua (ITCZ) kuendelea kusogea kuelekea kaskazini mbali na Tanzania. Joto la juu ya wastani liliendelea kuwepo katika eneo la kusini-mashariki mwa Bahari ya Hindi (karibu na Pwani ya Angola) hali iliyosababisha kudhoofu kwa pepo kutoka magharibi kuelekea katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2017

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa ilivyokuwa, maeneo mengi nchini yalikuwa makavu kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Namba 1. Hata hivyo, mvua chache na nyepesi za nje ya msimu wa mvua zilipatikana katika baadhi yamaeneo ya mikoa ya Lindi na Mara.




**Kielelezo 1**. Mwenendo wa mvua katika kipindi cha Juni11-20, 2017.

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2017

Katika kipindi cha Juni 11-20, 2017, mazao katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua yalikuwa katika hatua ya kukomaa. Zao la mahindi lilikuwa katika hatua ya kukomaa katika mikoa ya Geita, Mwanza, Mara, Manyara, Morogoro, Pwani, Tanga na Kilimanjaro. Katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua, hususan mikoa ya Kigoma,

Tabora, Rukwa, Katavi, Iringa, Mbeya, Njombe, Lindi, Ruvuma na Mtwara, zao la mahindi lilikuwa katika hatua ya kuvunwa. Upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo ulikuwa wa wastani katika maeneo mengi ya nchi, isipokuwa katika baadhi ya maeneo ya wilaya za Ngorongoro, Longido, Monduli na Simanjiro ambako hali ya maji na malisho ilikuwa duni kuliko maeneo mengine nchini.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2017

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vilipungua kiasi katika maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu inayoendelea.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2017

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyo kusini mwa Dunia (ST. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuimarika na hivyo kuimarisha mganadamizo mkubwa wa hewa wa Afrika Mashariki. Wakati huohuo, migandamizo ya kaskazini (Azores na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofu zaidi na hivyo kuendelea kuruhusu ukanda wa mvua wa ITCZ kusogea kaskazini mwa Dunia. Joto la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi na hii inatarajiwa kuendelea kusababisha mvua kidogo katika baadhi ya maeneo ya pwani ya kaskazini pamoja na yale ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Kwa upande mwingine joto la bahari la juu ya wastani hadi wastani linatarajiwa katika maeneo ya kusini magharibi mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola), hivyo kuendelea kuimarisha hali ya ukavu katika maeneo ya magahribi mwa nchi. Kuendelea kuimarika kwa migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa Dunia kunatarajiwa kusababisha kujitokeza kwa vipindi vya upepo mkali na ubaridi katika badhi ya maeneo ya nchi.

## HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2017

Maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuwa na hali ya ukavu pamoja na vipindI vya baridi. Hata hivyo mvua chache za nje ya msimu zinatarajiwa katika maeneo ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Mwanza, Mara, Geita, Simiyu na Shinyanga regions), nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara) na nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Iringa, Songwe na Mbeya). Vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa katika ukanda wa mwambao wa pwani (Mikoaya Tanga, Dar es Salaam, Morogoro, Lindi, Mtwara na Pwani) na mikoa ya kusini (Njombe na Ruvuma).

## ATHARI NA USHAURI KWA WAKULIMA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2017

Hali ya ukavu inayotarajiwa itasaidia kufanya shughuli za uvunaji na uhifadhi wa mazao.Wafugaji kote nchini wanashauriwa kuchukua hatua stahiki zikiwemo matumiziendelevu ya maji na malisho yaliyopo, pia wapate ushauri kutoka kwa maafisa mifugo katika maeneo yao.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2017

Kina cha maji katika mabwawa na mito vinatarajiwa kuendelea kupungua katika maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa pamoja na upepo mkali katika baadhi yamaeneo.Watumiaji wa maji wanashauriwa kutumia vizuri maji yaliyopo.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

*S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 Baruapepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet1_tz@meteo.go.tz*